Jina: …… Nambari ……..….....

Shule: ……...…. Sahihi: ……....

Tarehe: ……

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
UFAHAMU, MUHTASARI, MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMU JAMII
JULAI / AGOSTI 2013
MUDA SAA 2½

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA TRANSMARA MASHRIKI

Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari (K.C.S.E)

Kiswahili
Karatasi ya kwanza

Maagizo

- Jibu maswali yote katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha mtihani
- Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
- Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
- Mtihani una sehemu nne
- Mtihani huu una jumla ya alama 80
- Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	JUMLA	

1 UFAHAMU (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Maendeleo ya sayansi yamezua changamoto nyingi sana katika taaluma ya uundaji wa istilahi; msamiati au leksikoni katika nyanja mbalimbali maalumu ili kufanikisha mawasiliano. Hii ni changamoto kubwa si tu katika lugha ya Kiswahili bali pia lugha nyingine ulimwenguni. Suala la uundaji wa istilahi katika kswahili ni muhimu kwa sababu ya umaanifu wa lugha hii unaoendelea kupanuka kila uchao.

Kwa nini Kiswahili kiundiwe au kibuniwe istilahi? Kwa sababu pamezuka haja ya kushughulika nyanja ambazo zilikuwa hazishughulikiwi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa mtaalamu Joshua Fishman hatua ya kuiundia lugha istilahi ni ya kimakusudi ili kuiwezesha lugha hiyo kukidhi haja ya mawasiliano katika ufundi, utaalamu, elimu za juu na shughuli zinazohusu serikali na teknolojia.

Urasmi wa Kiswahili unamaanisha kwamba nyaraka zote za serikali zitahitajika kutafsiriwa kutoka kiingereza hadi Kiswahili.

Mtaalamu Ngugi wa Thiong'o tangu miaka ya 1970 amekuwa akikemea kasumba ya ukoloni ambayo anaamini imelemaza mifumo yetu kwa kutufanya tudharau tamaduni na lugha zetu.

Ngugi ametoa suluhisho rahisi sana katika swala linaloonekana kuwa tata mno. Mbona kila wakati tusiangalie mambo kwa kutumia mikabala ya kiafrika na kutatua matatizo yanayotukumba kwa kutafuta suluhisho za mumu humu mwetu? Ingawa Kiswahili kinajitahidi kupanua msamiati na istalahi zake bado kuna matatizo mengi. Kwanza hakuna vyombo mahususi au asasi maalum zilizotwikwa jukumu hilo nchini Kenya. Juhudi tunazoziona ni za watu binafsi na vyombo vya habari.

Pili hatuna taasisi inayoweza kutwikwa jukumu la kusanifisha istilahi hizo na labda kuzipiga muhuri kuwa ndizo zinazoidhinishwa kutumika katika mawasiliano. Juhudi za watu binafsi na vyombo vya habari kwa mfano Taifa Leo na shirika la Habari la Kenya (KBC) hasipaswi kupingwa, bali kuungwa mkono.

Hata hivyo, tahadhari ni lazima ichukuliwe ili kudhibiti mchakato mzima wa kubuni istilahi. Wataalamu wa Kiswahili ambao mchango wao katika kukubunia Kiswahili istilahi mpya unatambuliwa nchini Kenya ni pamoja na mzee sheikh Ahmad Nabhany wa Mombasa, profesa Rocha chimerah wa chuo kikuu cha pwani na profesa Kyallo Wamitila wa chuo kikuu cha Nairobi.

Kwa hiyo, Kenya inahitaji asasi maalumu inayoweza kutwikwa jukumu la kusawazisha na kusambaza istilahi zinazobuniwa na wataalamu hawa pamoja na vyombo vya habari. Mdahalo uliopo sasa ni iwapo watu binafsi wanaobuni istilahi za Kiswahili wamefuata utaratibu uliowekwa. Mtaalamu profesa Kibuka kiingi wa Uganda amependekeza kwamba , istilahi inayofaa zaidi lazima isheheni sifa za kimsingi ambazo zimefumbatwa kwenye nadhana ya PEGITOSCA.kwa hiyo, kila istilahi inayobuniwa ni lazima ikubalike kimataifa, iweze kunyambulika ili kuzalisha istilahi nyingine isiwe na matusi miongoni mwa sifa nyingine.

Kenya inahitaji asasi maalumu inayoweza kutwikwa jukumu la kusawazisha na kusambaza istilahi zinazobuniwa na wataalamu hawa pamoja na vyombo vya habari

(kimenakiliwa kutoka Taifa leo, tarehe 29mei, 2012)

Maswali

(a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

……

……

(b) Kwa nini ipo haja ya kuunda istilahi katika Kiswahili? (alama 2)

……

……

(c) Ni nini pendekezo la mtaalamu Ngugi Wa thiong'o la kuondoa utata na kasumba ya ukoloni? (alama 2)

……

……

(d) Zitaje changamoto zinazokabili kupanuliwa kwa msamiati na istilahi. (alama 4)

……

……

……

……

(e) Toa suluhisho kwa changamoto ulizozitaja kwa (d) kwa mujibu wa makala uliyosoma

(alama 2)

……

……

(f) Eleza maana ya maneno haya jinsi yalivyotumiwa; (alama 4)

(i) Leksikoni

……

……

(ii) Kasumba

……

……

(iii) Mchakato

……

……

(iv) Mdahalo

……

……

2. **MUHTASARI** (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Kiswahili ni lugha ambayo inakua na kuenea kila uchao. Imeenea kwa kasi hivi kwamba waliokuwa wameitweza wamelazimika kujifunza, kuizungumza na hata kuitumia katika maandishi

Lugha hii imetambuliwa kama mojawapo ya lugha za mawasiliano katika muungano wa Afrika. Magwiji wa Kiswahili wamechaguliwa kuunda msamiati mwafaka kutegemea mabadiliko ulimwenguni na kuingiza katika matumizi kupitia tarakilishi.

Mpango huu utakapofaulu, mtu ataweza kutumia tarakilishi akiwasiliana kwa Kiswahili. Juhudi hizi heri zizidi kupongezwa na nyingine kuimarishwa

Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili barani ni mojawapo wa hatua za kufanikisha juhudi hizi. Taasisi kama hiyo itatafiti historia ya lugha, mabadiliko yake na maenezi, msamiati wake na kulete usawa wa mazungumzo kwa Kiswahili miongoni mwa mambo mengine.

Kuweka lugha hii katika maandishi ni jambo litakalochangia kuimarisha lugha ya Kiswahili. Vitabu magazeti, na majarida yatakayolenga kiwango cha wasomaji yaandikwe na bei yake isiwe ghali mno ili wengi waweze kugharamia. Tanzu zote za lugha zizingatiwe

Lugha hii ifunzwe na kutahiniwa katika daraja zote za elimu. Lifanyapo hili, bila shaka lugha ya Kiswahili itaimarika. Uajiri wa wafanyikazi ukitambua ujuzi katika lugha hii hadhi yake itaimarika

Tafsiri ya kazi zilizoandikwa katika lugha mbalimbali zikifanywa katika Kiswahili, lugha hii itakua na kukita miziz kwingi ulimwenguni. Watu wengi watapata hamu ya kusoma kazi asilia na ile ya tafsiri yake.

Redio na magazeti ni vyombo muhimu katika kuwasiliana na kundi kubwa la watu kote duniani. Vyombo hivi vya mawasiliano kwa umma vikihimiza matumizi ya Kiswahili, bila shaka mchango mkubwa utaonekana katika kustawisha lugha hii. Vipindi maalumu matangazo, burudani, vizingatie matumizi ya Kiswahili

Mashindano kati ya shule na shule, nchi na nchi yakianzishwa na kuzingatiwa yanaweza kuimarisha Kiswahili pakubwa. Mashairi, mijadala, matokeo ya utafiti fulani, nyimbo, ngano na hadithi za kufunza umma ni njia za kuwezesha kufanyiwa mashindano kama hayo.

Mikakati hii na mingine ikizingatiwa itakuwa mbolea nzuri ya kukuza lugha ya Kiswahili.

Maswali

(a) Bila kubadilisha maana iliyokusudiwa fupisha aya mbili za mwanzo. (maneno 35 - 40) (alama 1 ya utiriko)

Matayarisho :

Nakala safi:

(b) Andika kwa muhtasari juhudi zinazofaa katika uimarishaji wa lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa makala haya.(maneno 70 -80) (alama 9; alama 2 ya utiririko)

Matayarisho:

Nakala safi:

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Andika neno la Kiswahili lenye muundo wa silabi mwambato wa konsontati tatau na irabu (KKK) (alama 1)

……

……

(b) Taja sauti nne zinazotamkiwa kwenye kaa kaa laini (alama 2)

……

……

……

……

(c) Bainisha vipengele vya kisarufi katika sentensi hii

Aliyekusamehea. (alama 3)

……

……

(d) Bainisha shamirisho katika sentensi: (alama 3)

Mwalimu atawasimulia wanafunzi hadithi kwa kipasa sauti.

……

……

(e) Eleza matumizi ya kiambishi ‘ni’ katika sentensi ifuatayo. (alama 4)

Halima ambaye ni rafiki yangu tangu utotoni alinitembelea nyumbani juzi.

……

……

……

……

(f) Tumia kiambishi ‘po’ kutunga sentensi itakayoonyesha (alama 2)

(i) Mahali

……

……

(ii) Wakati

……

……

(g) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia ‘O’rejeshi. (alama 2)

Malipo ambayo amepewa ni yale ambayo yanaridhisha.

……

……

(h) Kanusha sentensi hii. (alama 2)

Alipofika hotelini, aliomba chakula akapewa

……

……

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya vishale (alama 4)

Askari yule aliyekuwa mgeni alimpiga sana mfungwa.

……

……

……

……

(j) Andika kwa wakati ujao. (alama 2)

Ungalifanya kazi kwa bidii usingaliishi maisha ya dhiki.

……

……...

(k) Bainisha aina za vivumishi katika sentensi hii: (alama 4)

Mtoto wangu ni huyu aliyevaa mashati mawili mapya

……

……

……

……

(l) Andika ukubwa wa: (alama 2)

Kijana alichukua mbuzi na ng'ombe

……

……

(m) Kosoa sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Chai zilizoandaliwa na mama zimesheherekewa

……

……(

(ii) Hizi ni vikombe za kukunywia chai.

……

……

(n) Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya umoja (alama 2)

(i) Huko kusoma kwao kuzuri kutawapendeza walimu

……

……..

(ii)Hayo matofali ni mazuri sana, yatatufa.

……

……

(o) Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi hivi:- (alama2)

(i) Tiba

……

……

(ii) Zaa

……

……

(p) Andika sentensi ifuatayo kwa usemi halisi (alama 3)

Mwalimu alisema alikuwa amefurahishwa na yote aliyoyaona

……

……

4. ISIMU JAMII (alama 10)

(a) Hujambo bwana: you look familiar, have we ever met before……sijui nilikuona wapi?

(i)Mtindo huu wa kutumia lugha unaitwaje? (alama 2)

……

……

(ii) Eleza sababu tatu zinazopelekea watu kutumia mtindo huu wa lugha (alama 6)

……

……

……

……

(iii) Pendekeza njia mbili za kuondoa mtindo huu wa lugha. (alama 2)

……

……

ANSWERS:
Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy
NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs